

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO  
SHULE YA SEKONDARI UDZUNGWA  
S. L. P. 1693- IRINGA**

*Mawasiliano:*  
0762738564  
*Au*  
0764921641



Jina la mwanafunzi .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UDZUNGWA  
WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA MWAKA 2021**

**UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka 2021. Shule ya sekondari Udzungwa iko umbali wa kilometra 62 Kusini Mashariki mwa mji wa Iringa. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 09/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021. Baada hapo unaweza kupoteza nafasi yako.

**1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.1 SARE ZA SHULE**

**(a) WAVULANA**

- ❖ Suruali mbili za khaki, sampuli ya kitambaa imeambatanishwa kwenye fomu hii. Suruali iwe na malinda mawili kila upande na nchi 17 za mzingo wa chini.
- ❖ Mashati meupe mawili ya mikono mirefu
- ❖ Tai nyeusi
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba jozi mbili
- ❖ Soksi nyeusi jozi mbili
- ❖ Trakisuti nzito pana nyeusi yenyenye mstari mweupe pembeni jozi mbili
- ❖ Sweta la shule la brauni jozi moja.
- ❖ Suruali mbili damu ya mzee kwa ajili ya kuvalaa mwanafunzi akiwa kazi za nje ya darasa
- ❖ Tisheti ya Kahawia.
- ❖ Sweta jeusi lenye kofia kwa ajili ya mwanafunzi kujikinga baridi

**(b) WASICHANA**

- ❖ Sketi mbili za darasani zenyе marinda nane ya kupanga (malinda manne mbele na manne nyuma), mkanda nchi mbili. Sampuli ya kitambaa imeambatanishwa pamoja na fomu hii. Mfuko upande wa kushoto.
- ❖ Mashati meupe mawili mikono mirefu
- ❖ Tai fupi ya kijani kitambaa kama cha sketi
- ❖ Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu jozi mbili
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili
- ❖ Sweta la shule la brauni jozi moja.
- ❖ Trakisuti nyeusi pana nzito yenyе mstari mweupe pembeni jozi mbili
- ❖ Tisheti ya Kahawia.
- ❖ Shamba dress (sketi) kitambaa cha damu ya mzee malinda nane (manne mbele na manne nyuma) na mkanda nchi mbili.
- ❖ Hijabu rangi nyeupe iishie kwenye viwiko vya mikono na ifunike kifua.
- ❖ Sweta jeusi lenye kofia kwa ajili ya kujikinga baridi

**NB: Ni muhimu kuzingatia sare ya shule kwa sababu mwanafunzi hataruhusiwa kuja na nguo nyingine zaidi ya hizo zilizo ainishwa hapo juu.**

**1.2 MASOMO**

Uwapo shule pamoja na mambo mengine utakayojifunza utasoma masomo yafuatayo:

❖ His  
aba  
ti  
❖ Kii  
nge  
rez  
a  
❖ Jio  
gra  
fia  
❖ Kis  
wa  
hili  
❖ Eli  
mu  
ya  
viu  
mb  
eha  
i  
❖ Eli  
mu  
ya  
ura  
ia  
❖ Fiz  
ikia  
❖ Ke  
mia  
❖ His  
tori  
a  
❖ Kil  
im  
o

Masomo yote yatafundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili. Hivyo mwanafunzi atatakiwa kujifunza lugha ya Kiingereza kwa bidii zaidi awapo shulenii ili aweze kuyamudu masomo hayo.

**NB: Lugha kuu ya mawasiliano wakati wote uwapo shulenii ni lugha ya Kiingereza.**

### **1.3 MAHITAJI YA KITAALUMA**

- ❖ Mkebe wa vifaa vya hesabu (Mathematical set/Compax box)
- ❖ Daftari kubwa 15(Counter books quire 3)
- ❖ Vitabu vya rejea kwa ajili ya kujisomea (Review Books)
- ❖ Kalamu, rula, ufuto, penseli, na vifaa vingine vya kitaaluma

**USHAURI:** Mzazi unashauriwa kununua walau kitabu kimoja kimoja kwa kila somo pamoja na kamusi ya Kiingereza kwa Kiingereza.

## **2.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

**2.1** Shule ina endeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, ina zingatiwa miongozo yote inayo tolewa na Wizara Ya Elimu, Sayansi, Teknologia na Ufundu yenye dhamana na elimu nchini na ofisi ya Rais (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ya fuatayo mara baada ya kufika shulenii:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyininge utakazo pewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvalaa sare ya shule wakati wote unapo takiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote (daily routine) na
- i) Kutunza mali za umma, za kwako na za mwenzio.

### **2.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, Cocane, mirungi, kuberi nk.
- e) Kupiga au kupigana
- f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma, na za wenizio
- g) Kudharau bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito au kuwa na mimba
- i) Kuoa au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki mgomo kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

- m) Kuwa na simu ya mkononi( **mwanafunzi asije na simu wala kuwekeza kwa mtumishi yoyote simu, line, chaja au memory card**).

**NB:** Utaratibu wa mawasiliano kwa wanafunzi wote wataelekezwa wafikapo shulenii. Ni marufuku mwanafunzi kufanya mawasiliano kwa mzazi/mlezi nje ya utaratibu uliowekwa na uongozi wa shule.Kinyume chake hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzi atakayevunja utaratibu huo.

### **3.0 MKATABA WA KUKUBALI NAFASI HII.**

- a) **(Ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi)**

Mimi.....mzazi/mlezi  
nakubali/nakataa(jina la mwanafunzi).....ajiunge  
na Shule ya Sekondari Udungwa na nitampa vifaa na mahitaji kama ilivyoagizwa.  
Vile vile naahidi kuwa nitatoa ushirikiano kwa walimu katika kumlea mtoto hadi  
hapo atakapo hitimu masomo yake.

Anuani.....namba ya simu.....

- b) **(Ijazwe na mwanafunzi)**

Mimi.....nakubali/nakataa kutii sheria na  
kanuni za shule na maagizo yote yatakayo tolewa na mkuu wa shule, walimu na  
mtu ye yeyote mwenye mamlaka.

Sahihi..... Tarehe.....

**MOTO WA SHULE NI “THE ROOTS OF EDUCATION ARE BITTER  
WHILE FRUITS ARE SWEET”**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....  
**ASHERI MBOGORA MANYAMA  
MKUU WA SHULE**

### **4. MEDICAL EXAMINATION FORM**

**Ijazwe na daktari wa hospitali au kituo cha afya na sio zahanati.**

Please examine the above mentioned student on the following:

- (a) Eye problem, normal ..... Affected .....
- (b) Ear, normal ..... Affected .....
- (c) Pregnancy test .....
- (d) Blood test .....
- (e) Urinalysis .....
- (f) Stool .....
- (g) Any chronic disease/s .....

I hereby certify that, the examined student is fit/unfit to be registered for the above mentioned course as far as his/her health is concerned.

Name.....Signature.....Title.....  
Date.....